

# Mazingira na Udhibiti Taka Ngumu

## I. Utangulizi

Halmashauri kupitia Idara ya Mazingira na Udhibiti taka Ngumu inaendelea kusimamia utunzaji na udhibiti wa uharibifu wa mazingira ndani ya wilaya.

## II. HALI YA WATUMISHI

Idara ina jumla ya watumishi 2 wa Idara ya Mazingira na Udhibiti Taka Ngumu.

NA	KADA	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU
1	MKUU WA IDARA	1	1	0
2	MAAFISA MAZINGIRA	5	1	4

*Chanzo: Idara ya Utumishi na Utawala, 2018*

## III. MAJUKUMU YA IDARA KWA UJUMLA

Idara inawajibika kutekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo

- Kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa mazingira kwenye eneo zima la Halmashauri ya Bukombe
- Kushauri Menejiment na Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri kuhusu masuala yote ya mazingira
- Kukuza weledi kuhusu ulinzi wa mazingira na uhifadhi maliasili kwenye Halmashauri
- Kukusanya na kusimamia taarifa kuhusu mazingira na matumizi ya maliasili ndani ya Halmashauri
- Kuandaa taarifa za mihula kuhusu hali ya mazingira ndani ya Wilaya
- Kufuatilia maandalizi, mapitio na vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa ajili ya uwekezaji wa ndani wa miradi mbalimbali
- Kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira;
- Kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa mazingira.
- Kutoa (disseminate) Elimu ya Hifadhi ya Mazingira kwa wadau mbalimbali.
- Kushiriki katika kuandaa mpango kazi na Bajeti.
- Kushiriki katika tafiti zinazohusu usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.
- Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa.

- Kufanya ukaguzi wa usafi katika maeneo ya mji, mtaa, kaya kama sheria, kanuni na miongozo inavyoelekeza.
- Kuhimiza na kuratibu zoezi la ukusanyaji wa taka ngumu na kuzitupa kwenye maeneo tengwa Mfano.dampo.
- Kusimamia uundwaji wa kamati za mazingira na kuziimarisha katika ngazi zote za kiutawala

#### **IV. MIKAKATI YA IDARA**

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kupitia Idara ya Mazingira na Udhibiti Taka Ngumu imejiwekea mikakati mbalimbali ili kuboresha utunzaji wa mazingira na Udhibiti taka ngumu. Mikakati hiyo ni pamoja na;-

1. Kuhakikisha kwamba elimu juu ya Hifadhi ya mazingira na afya ya jamii kwa wadau mbalimbali inafanyika mara kwa mara ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la uharibifu wa mazingira na utupaji hovywa wa taka ngumu katika Wilaya.
2. Kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa mazingira no 20 ya 2004 na marekebisho yake ya 2016 dhidi ya waharibifu wa mazingira, na ukiukwaji wa sheria ya afya ya jamii na 1 ya 2009 dhidi ya wale wote wanaoenda kinyume na kanuni, taratibu na miongozo ya afya ya jamii. Na sheria ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya wilaya ya Bukombe GN.190 la tarehe 21/6/2013.
3. Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa kama maeneo yenye chepechepe za maji (Aridhi oevu), kandokando mwa kingo za mito, milima ya hifadhi ya jamii, na maeneo mengine yenye thamani mbalimbali ya uhifadhi.
4. Kuboresha taaluma ya watumishi pamoja na maslahi.
5. Kuandaa mikakati na mipango mbalimbali ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira kama programu za upandaji miti.
6. Kufuatilia maandalizi, mapitio na vibali vya Tathmini za athari za mazingira zina fanyika kwa miradi mikubwa ya uwekezaji kama vile miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, Mashule, Minara, uchimbaji wa madini na pia wachimbaji wadogo wa madini kuhakikisha wa mipango ya Ulinzi wa mazingira (EPP) na mipango ya usimamizi wa mazingira yaani (EMP) kwa

mujibu wa sheria ya usimamizi wa Mazingira na 20 ya 2004 na sheria ya madini na 14 ya 2010.

7. Kuunda kamati za kuhifadhi mazingira kuanzia ngazi ya vijiji, kata na wilaya pamoja na klabu za mazingira mashuleni.
8. Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi kwa viongozi, watendaji na kamati za Mazingira.
9. Kuandaa maandiko mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa mazingira na afya ya jamii ndani ya Wilaya ya Bukombe
10. Kusimamia zoezi la Usafi wa Mazingira kwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi

#### **V. CHANGAMOTO ZA KIMAZINGIRA**

- i. Uharibifu wa Mimiti ya asili (Deforestation / Forest degradation)
- ii. Uharibifu wa Mifumo ya ikolojia ya Maji (River and Wetland Degradation) Mifumo na Vyanzo
- iii. Uharibifu wa Ardhi (Land Degradation)
- iv. Kupotea kwa Bionuai ( Loss of Biodiversity)
- v. Uharibifu na Uchafuzi wa Mazingira
- vi. Mabadiliko Tabianchi (Climate Change)

#### **VI. SHINIKIZO (PRESSURE)**

- a. Kasi ya uharibifu wa Mazingira inasababishwa na utupaji wa taka ovyo,
- b. ukosefu wa madampo ya kisasa,
- c. Kilimo cha Kuhamahama, upanuzi wa mashamba,
- d. Matumizi makubwa ya nishati ya kuni na mkaa, mifugo mingi kupita kiasi,
- e. uchimbaji holela wa madini, ukataji miti kwa ajili ya kuni, mkaa, nguzo na mbao,
- f. ujenzi wa miundombinu ya barabara unaoambatana na ufyekaji miti na misitu ovyo,

Haya ndiyo mashinikizo makubwa katika wilaya ya Bukokombe yanayosababisha kasi kubwa ya uharibifu wa Mazingira.

## VII. HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA/ MIKAKATI (RESPONSE)

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe imechukua na inaendelea na mikakati na mipango endelevu ifuatayo:-

- Kuondoa watu waliovamia Misitu kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo, uchimbaji wa madini na ufugaji, (eviction)
- Kutoza faini kwa wavamizi wa Misitu na wachafuzi wa mazingira mjini na vijijini,
- Kuhamasisha upandaji miti, utunzaji misitu na ufugaji nyuki wa kisasa kwenye misitu
- Kuhamasisha jamii na kutoa elimu juu ya kilimo cha kutumia makinga maji na matumizi ya mbolea ya asili,
- Kuhamasisha jamii na kutoa elimu kwa jamii juu ya utunzaji wa mazingira; kusimamia utekelezaji wa sheria ya Misitu 2002 na Usimamizi wa sheria ya Mazingira 2004 na kanuni zake,
- Kushirikisha wadau mbalimbali muhimu katika kusimamia utunzaji wa mazingira,
- Kuandaa miongozo ya kuzuia uharibifu wa Misitu katika maeneo ya uwekezaji,
- kuendelea na kampeni ya upandaji miti million 1.5 kila Mwaka na kuhifadhi Misitu ya asili,
- Kuhakikisha kuwa miradi yote inafanyiwa EIA na kuandaa mpango wa usimamizi wa mazingira (EMP) na EPP Mipango ya ulinzi wa Mazingira katika miradi ya wachimbaji wadogo kwa kuzingatia sheria zilizopo.
- Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye maeneo ya yote ya wilaya.
- Kuhamasisha jamii na kuendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati mbadala, majiko banifu na vyanzo mbadala vya kipato rafiki wa mazingira (Ufugaji samaki, nyuki, kuku, kilimo cha matunda).
- Kusimamia zoezi la Usafi wa Mazingira kwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.